

Mabadiliko ya Tabia Nchi, Kilimo na Kupunguza Umasikini

kuwaweka wakulima
wadogo kwenye sera na
utendaji





Wakulima wa kijiji cha manchali B wilayani chamwino wakiwa katika mafunzo ya namna ya utengenezaji wa vitalu vya miti.)

Mabadiliko ya Tabia Nchi, Kilimo na kupunguza Umasikini (CCAPA)

CCAPA ni mradi unaowasaidia wakulima katika kupigania sera na mikakati ambayo huwasaidia wakulima wadogo kuboresha maisha yao kwa kuasili kilimo endelevu na mfumo wa utunzaji wa ardhi na mali asili..

Utangulizi

Wakulima 25 wakiwemo wanawake 12 kutoka katika vijiji vitano wilayani Chamwino walipatiwa mafunzo, kwa muda wa siku tatu, kuhusu Ushawishi na utetezi. Wakulima hao walainisha mambo kadhaa muhimu na mawazo yao kuhusu kilimo endelevu. Timu ya Utetezi ilihusisha wawakilishi wa wakulima kutoka katika vijiji vitano. Kila kijiji kilitoa wawakilishi watano, hivyo kufanya jumla yao kuwa 25. Aidha wakulima 258 (kati yao 154 wakiwa wanawake), kutoka katika vijiji hivyo, walishirikishwa kwenye

mikutano kwa ajili ya kupitia, kuboresha na kuthibitisha maoni yao na ujumbe wao kabla ya kuwasilishwa kwa viongozi wa jamii na watoa maamuzi.

Maoni ya Wakulima Wa Chamwino

- » Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya pamoja na Sheria Ndogo za vijiji/wilaya havikuweza kujishughulisha kikamilifu na kusaidia teknolojia za kilimo mahsusini cha wakulima wadogo dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi (C3S).
- » Utekelezaji dhaifu wa sheria na miongozo iliyowekwa ni jambo la kawaida katika ngazi zote kama vile kutoka ngazi ya kijiji kwenda ngazi ya wilaya. Teknolojia za kilimo za C3S hazikupewa kipaumbele na/au hazitekelezwi katika ngazi ya kijiji na wilaya.



Afisa Kilimo wa TOAM Ndg. Bakari Mongo akiwa na viongozi wa wakulima wa kijiji cha mahama.)

Kilimo Mahsusini Dhidi ya Mabadiliko Ya Tabia Nchi (C3S) Ni Nini?

C3S (kilimo mahsusini) kinahusisha mbinu endelevu kwenye ikolojia kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji wakati huo huo ikipunguza utoaji wa gesi kutoka katika chumba maalum cha kuzalishia mimea. Hii inajumuisha:

- Mbinu za kilimo Bora - kupanda, kupalilia na kupunguzia miche
- Utumiaji wa mbegu bora zenyе ukinzani dhidi ya ukame - Aina za mbegu zinazochamvushwa/ Mbegu za daraja la Kudhaminiwa Ubora
- Utumiaji wa wanyamakazi na zana za kulimia - kutayarisha shamba kwa ajili ya kupanda
- Utunzaji wa rutuba ya udongo - kutumia samadi, kuchanganya mimea jamii ya mikunde
- Utunzaji wa unyevu kwenye udongo - kutumia kilimo cha kontua

- Udhibiti wa mmomonyoko wa udongo - kujaza makorongo, fanya juu, fanya chini
- Uongezaji thamani kwenye mazao na masoko - kwa ajili ya kuongeza kipato cha mkulima.

Wakulima wa Chawino Wanawataka Viongozi Kuzingatia Yafuatayo:

1. Kuhakikisha kuwa teknolojia za C3S zinaingizwa kwenye mipango ya kilimo na sheria ndogo za vijiji
2. Kuweka mkazo kwa ajili ya upokeaji/vasilishaji mpana na usambazaji wa teknolojia za C3S
3. Kuhakikisha kuwa teknolojia za C3S zinaingizwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo na sheria ndogo za wilaya.

Mabadiliko ya Tabia Nchi, Kilimo na Kupunguza Umasikini (CCAPA) ni jitihada za pamoja kati ya vyama vine vya hiari/jamii vilivyojikita katika kuboresha uwajibikaji na uzoefu maalum katika kilimo, mabadiliko ya tabia nchi na utunzaji wa misitu. Mashirika hayo ni TFCG, MJUMITA, TOAM na ANSAF. Jitihada hizo zinalenga kupeleka Tanzania kwenye njia ya maendeleo ya kilimo ili kupunguza umasikini na gesi zinazozalishwa kwenye vyumba malum vya kukuzia mimea.

Mradi huu unafadhliliwa na Shirika la Maedeleo la Kimataifa la Waingereza (DfID) na Shirika la kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA) kuitia AcT, Mpango wa Uwajibikaji Tanzania.

